



USAID

KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



Mwandishi wa Habari wa Ice FM Ms Consolata Damian Motto (aliyesimama kulia) akiandaa kipindi cha redio kinachohusu wanawake na vijana. Boresha Habari inasaidia maudhui ya vyombo nya habari shirikishi.

Picha na: Temigunga Mahondo. Mkufunzi wa Vyombo nya Habari wa Internews

TANZANIA BORESHA HABARI

Mradi wa Boresha Habari wa USAID unasaidia Kuimarisha mazingira yilio wazi, na jumuishi ambapo vyombo nya habari na asasi za kiraia hutoa habari sahihi na zilizokuwa na usawa ambazo zinakuza ushiriki, ujumuishaji, na uwajibikaji. Lengo kuu la mradi huu ni kuwashirikisha na kuwawezesha wanawake na vijana. Lengo ni kuinua sauti zao, ushawishi, na masuala mbalimbali katika nyanja ya umma kama wazalishaji na watumiaji wa habari.

Mradi utafanya kazi kufanikisha malengo ya kimkakati manne:

1. Kuboresha mazingira ya kuviwezesha vyombo nya habari kufanya kazi kwa usalama na umakini nchini
2. Kuimarisha taaluma ya wadau wa vyombo nya habari na waandishi wa habari kutoa habari zenyenye ubora wa hali ya juu na zilizothibitishwa na zilizo na takwimu sahihi
3. Kuongeza uwezo na uimara wa vituo nya redio za jamii kutoa habari sahihi, zisizo na ubaguzi, na zenyenye manufaa
4. Kuimarisha uwezo wa asasi za kiraia kuweza kutumia vyema vyombo nya habari kuwasiliana kwenye masuala muhimu

Boresha Habari itawezesha vyombo nya habari nya Tanzania na asasi za kiraia kukuza uhuru wa kujieleza na uwezo wa kupata habari. Mradi unakusudia kuongeza habari zilizo huru, za kuaminika na zenyenye takwimu sahihi kwa jamii na kuwashirikisha raia katika majadiliano ya umma yaliyo na habari zilizothibitika juu ya masuala muhimu ya kila siku. Kipaumbele kitakuwa kufanya kazi na vituo nya redio nya jamii vilivyo chaguliwa nchini kote kuongeza uwezo wao wa

kitaalam wa kutoa habari zenye ubora na kuboresha biashara zao na uimara wa kifedha. Kwa kuongezea, kwa juhudii zote, wanawake na vijana watashirikishwa na kuwezeshewa ili kupaza sauti zao katika vyombo vya habari.

MAFANIKO MPAKA SASA

- Zaidi ya waandishi wa habari 200 katika mikoa tisa warmepokea mafunzo ya msingi na ya kati kuhusu kuzalisha habari kwa kiwango chenye ubora, jinsi ya kuboresha tovuti na mitando ya kijamii, jinsi ya kupaza sauti za wanawake na vijana katika vipindi vyao na jinsi ya kuboresha usawa katika ripoti zao.
- Kuunda mtando usio rasmi wa mameneja kutoka vituo 20 vya redio za jamii katika mikoa tisa, na kuwasaidia kuandaa rasimu za biashara na kubaini zaidi ya masoko 100. Vituo hivi vimeongeza uwezo wao wa kitaaluma na kuboresha uwezo wao wa uenezi kwa vyombo vipya vya Habari na vifaa vya mawasiliano.
- Imewapatia wadau wa vyombo vya habari fursa za kawaida - kama majadiliano pande zote jijini Dar es salaam na mafunzo ya kitaifa - kujadili na kujifunza juu ya sheria mpya ya vyombo vya habari inavyoathiri utendaji wa vyombo vya habari kila siku.
- Kuunda mtando wa waandishi waandamizi wanawake jijini Dar es salaam waliopata mafunzo na ushauri wa mara kwa mara ili kuboresha nafasi zao za kazi kwenye vyombo vya Habari.
- Iliunga mkono warsha 18 zinazoweza mwaka 2018 ambazo zilikusanya pamoja vyombo vya habari na asasi za kiraia kushirikishana taarifa, kujadili mwenendo wa ndani, na kuongeza uhamasishaji juu ya masuala muhimu kuititia vyombo vya habari.
- Kuanzisha ushirikiano na Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano (SMJMC), Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania jijini Mwanza, na Chuo cha Uandishi wa Habari cha Zanzibar na, mwaka 2018, ilifadhili wanafunzi wa uandishi wa habari kutoka vyuo vikuu hivi kuhudhuria mafunzo kwa vitendo ya wiki sita baada ya kuhitimu chuo kikuu.

BAJETI Dola za Marekani milioni 9.7

MUDA

Agosti 2017 – Agosti 2022

MAENEKO YA MRADI

Dar es Salaam, Zanzibar, Iringa, Mbeya, Morogoro, Arusha, Manyara, Dodoma, Tanga, Mtwara, Mwanza, na Kigoma.

MTEKELEZAJI

Internews
FHI 360

WASHIRIKA WAKUU

Baraza la Habari la Tanzania
JamiiForums
International Center for Not-for-Profit Law (ICNL)
GeoPoll – Mobile Accord, Inc.
Media Institute of Southern Africa (MISA)
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

MAWASILIANO YA USAID

Theodore Glenn
Afisa Mwakilishi wa Mradi
+255 22 229 4508
tglen@usaid.gov

MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI

Angela Nicoara
Mkuu wa Mradi
+255 742 378 388

KWA TAARIFA ZAIDI

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania